**UBALOZI WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**P.O. Box 36302,**
**Ibn Bathouta Street No – 591**
**Onaiza – 65**
**Al Dafna , Doha, Qatar**
**Tel: +974 40360860, Fax: +974 40294067**
**E-mail: doha@nje.go.tz**
**https://www.qa.tzembassy.go.tz**

صندوق البريد ٣٦٣٠٢
شارع ابن بادودا رقم الشارع 591
العنيزة, الدفنة، الدوحة, قطر
تليفون: +974 40360860
فاكس : +974 40294067
البريد الإلكتروني: doha@nje.go.tz
https://www.qa.tzembassy.go.tz

**سفارة جمهورية تنزانيا المتحدة**
**EMBASSY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**Kumb. Na. CNAE 622/729/01/D/65** **26 Februari, 2025**

Katibu Mkuu,
Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki,
Mji wa Serikali – Mtumba,
S.L.P. 29333,
**40466 DODOMA.**

**YAH: TAARIFA YA MAZUNGUMZO KATI YA MHESHIMIWA HABIBU AWESI MOHAMED, BALOZI WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA NCHINI QATAR NA MHE. ABDULLAH BIN KHALAF BIN HATTAB AL KAABI, KATIBU MKUU, WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA TAIFA LA QATAR**

Tafadhali husika na kichwa cha habari hapo juu.

1. Mnamo tarehe 26 Februari, 2025 Balozi wa Jamhuri ya Muungano waTanzania nchini Qatar Mheshimiwa Habibu Awesi Mohamed alikutana na kufanya mazungumzo na Mheshimiwa Abdullah Bin Khalaf Bin Hattab Al Kaabi, Katibu Mkuu, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Taifa la Qatar. Mazungumzo hayo yalifanyika kufuatia ombi lililowasilishwa na Mheshimiwa Balozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Qatar na kufanyika katika Makao Makuu ya Wizara hiyo mjini Doha, Qatar.

2. Lengo kuu la mazungumzo hayo pamoja na masuala mengine lilikuwa ni kuimarisha ushirikiano katika masuala ya ulinzi na usalama kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Taifa la Qatar. Aidha, malengo mahsusi ya mazungumzo hayo yalikuwa ni:-

i. Uwezekano wa kusaini Hati ya Makubaliano ya masuala ya Zimamoto na Uokoaji na *Ambulance* ***"Memorandum of Understanding in the Field of Firefighting, Rescue and Ambulance"***;

*ii.* Kukamilisha na kusaini wa Usajili na Utambuzi wa watu ***"Memorandum of Understanding in the Field of Registration and Identification of Persons";***

*iii.* Uwezekano wa Tanzania kupatiwa mwaliko wa kushiriki katika maonesho ya *"Military Police Exhibition (Milipol)" na "Doha International Maritime Defence Exhibition (DIMDEX)" na*

iv. Uwezekano wa kushirikiana na Serikali ya Qatar katika kuandaa mashindano ya AFCON 2027 yanayotarajia kufanyika nchini Tanzania;

v. Maombi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhusu uwezekano wa Mkuu wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM) kwa upande wa Zanzibar kufanya ziara nchini Qatar ili kuonana na mwenzie upande wa Qatar;

3. Katika mazungumzo hayo, Mheshimiwa Kaabi, alitumia fursa hiyo kumkaribisha Mhe. Balozi Awesi katika Ofisi hizo na kumfahamisha masuala yafuatayo: -

a) Wizara inakaribisha ushirikiano wa vyombo vya usalama na tayari barua kuhusu ushirikiano huo ilitumwa kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania toka 2003.

b) Wizara iko tayari kutoa ushirikiano na kusaidia katika maandalizi ya AFCON 2027, hivyo upande wa Tanzania uandae rasimu ya Hati ya Makubaliano kuhusu ushirikiano huo;

c) Wizara haina taarifa ya uwepo wa hati ya Makubaliano katika masuala ya usajili na utambuzi wa watu kati ya pande mbili hizi;

d) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Qatar haijapokea rasimu ya Hati ya Makubaliano kuhusu masuala ya zimamoto na uokoaji na Ambulace kutoka upande wa Tanzania;

e) Ubalozi ukajiridhishe kuhusu Wizara sahihi ya kuwasilisha ombi la ziara ya Mkuu wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kwa upande wa Zanzibar kama Wizara ya Mambo ya Ndani au Wizara ya Ulinzi nchini Qatar kwa hatua zinazofuata.

4. Kwa kuzingatia hayo, pande mbili hizo zilikubaliana masuala yafuatayo:-

- Mwaliko kwa vyombo vya Ulinzi na Usalama vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania utatolewa ili viweze kushiriki katika maonesho tajwa hapo awali;
- Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwasilisha rasmi rasimu za Hati za Makubaliano za masuala ya Zimamoto, Uokoaji na Ambulance na ile ya usajili

na utambuzi wa watu ili ziweze kukamilishwa na kupangiwa tarehe ya kutiwa sahihi mapema iwezekavyo;

- Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwasilisha rasimu ya hati ya makubaliano kuhusu ushirikiano na taifa la Qatar katika maandalizi ya AFCON 2027;
- Maombi rasmi yawasilishwe kwenye Wizara husika ili kuharakisha ziara ya kiongozi huyo wa ulinzi na usalama Zanzibar.

5. **Maoni na Mapendekezo ya Ubalozi**:

a) Ubalozi kufuatilia kwa wakati mwaliko wa ushiriki wa vyombo vya ulinzi na usalama katika maonesho ya *"Military Police Exhibition (Milipol)" na "Doha International Maritime Defence Exhibition (DIMDEX)"* nchini Qatar;

b) Ubalozi kuwasilisha kwa mara nyingine tena rasimu za Hati za Makubaliano kuhusu masuala ya zimamoto, uokozi na ambulance pamoja na usajili na utambuzi katika Wizara ya Mambo ya Nje nchini Qatar ili kuharakisha utiaji sahihi wa hati husika;

c) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuwasilisha kwenye mamlaka husika pendekezo la ushirikiano na Serikali ya Qatar kuhusu kuandaa kombe la AFCON 2027 kwa upande wa Tanzania; ikiwa ni pamoja na kuandaa rasimu ya hati ya makubaliano( MoU); na

d) Ubalozi kuwasilisha rasmi maombi ya ziara ya kiongozi wa masuala ya ulinzi na usalama wa majini kwenye Wizara husika baada ya kufanya mawasiliano na kujiridhisha na mamlaka ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Tunatanguliza shukrani zetu kwa ushirikiano wako wa dhati na wa siku zote.

Maryam H. Mrisho
**Kny: BALOZI**

EMBASSY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
DOHA QATAR

Nakala: - - Katibu Mkuu,
Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi,
Mji wa Serikali - Mtumba,
S.L.P. 2916,
**40483 DODOMA**.

- Mkurugenzi,
Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki,
Afisi ya Zanzibar,
S.L.P. 296,
**ZANZIBAR**.